

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA

Anuani ya Simu “MKUUPOLISI”  
Simu: (026) 2323585  
Fax Na: (026) 2323586



Ofisi ya Inspekta Jenerali wa Polisi,  
Makao Makuu ya Polisi,  
4 Mtaa wa Posta,  
S.L.P 961,  
40483 DODOMA.

03/09/2021

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Ndugu Wanahabari,**

Tarehe 30/08/2021 katika vyombo vya habari zilitolewa taarifa zenye malalamiko dhidi ya Polisi wilaya ya Handeni, kwamba wamekuwa na tabia za kuwashika shika wanawake au mabinti katika maungo yao bila ridhaa yao na kuwataka kimapenzi kwa nguvu na pale wanapokataa huwatafutia makosa na kuwaweka mahabusu.

Taarifa hiyo iliambatana na taarifa ya Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Handeni ikiongozwa na Mhe. Mkuu wa Wilaya hiyo baada ya kufika eneo la tukio na kuanza kufanyia kazi malalamiko hayo kwa mujibu wa taratibu zilizopo. Pia Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga alianza kuyafanyia kazi malalamiko hayo na alitoa taarifa yake ya awali kwa vyombo vya habari.

**Ndugu Wanahabari,**

Jeshi la Polisi Makao Makuu baada ya kuona uzito wa malalamiko hayo, lilituma afisa wake kwenda wilayani humo kufanyia kazi malalamiko hayo ili kupata ushahidi wa kweli na kuona ni nini hasa kilichotokea.

Aidha, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi hasa wale wenye taarifa za kweli, waliotendewa na walioshuhudia vitendo hivyo vikifanyika wasisite kujitokeza kutoa maelezo yao ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Jeshi la Polisi linaendelea kusisitiza kuwa hakuna mtu aliyejuu ya sheria na endapo ushahidi utathibitisha kwamba hayo yaliyolalamikiwa na kurushwa kwenye vyombo vya habari ni ya kweli basi hatua stahiki zitachukuliwa na kama ni askari Polisi taratibu zetu ziko wazi atashitakiwa kijeshi na kufikishwa mahakamani kulingana na sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu.

Wananchi waendeleo kutulia wakati hatua hizo zikichukuliwa. bila kumuonea mtu muhali au kumuonea mtu yeyote yule.

Kwa vile Kamati ya Usalama ya Wilaya walishaanza kufanyia kazi malalamiko hayo kupitia kwao wale waliotendewa na kushuhudia wasisite kufika na kutoa ukweli wao.

Asanteni kwa kunisikiliza.

**Imetolewa na:**

David A Misime

**Msemaji wa Jeshi la Polisi**

Makao Makuu ya Polisi,

Dodoma, Tanzania.

[www.polisi.go.tz](http://www.polisi.go.tz)

[www.twitter.com/tanpol](https://www.twitter.com/tanpol)

[www.facebook.com/tanpol](https://www.facebook.com/tanpol)